

**Wakuu wa Mashtaka Mikoa,
Wakuu wa Mashtaka Wilaya,
Waendesha Mashtaka Viongozi,
Wakuu wa Vyombo Vya Uchunguzi nchini.**

**YAH: MWONGOZO WA MKURUGENZI WA MASHTAKA NAMBA 1 WA MWAKA
2022 KUHUSU UFUNGUAJI WA MASHTAKA NA UKAMILISHAJI WA UPELELEZI
WA KESI ZA JINAI**
(Chini ya kifungu cha 18(1) cha Sheria ya Mashtaka, Sura ya 430)

**SEHEMU YA KWANZA
UTANGULIZI**

1. Utaratibu wa kufungua, kuendesha na kusimamia uendeshaji wa kesi za jinai nchini unaongozwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sura ya 2, Tangazo la Serikali Na. 49 la mwaka 2018, Sheria ya Mashtaka, Sura 430, Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai, Sura ya 20 pamoja na Waraka na Miongozo mbalimbali iliyopo, unasimamiwa na Mkurugenzi wa Mashtaka.
2. !bara ya 59B (4) (a)(b) na (c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kifungu cha 8 cha Sheria ya Mashtaka vinatamka misingi mitatu ambayo inamuongoza Mkurugenzi wa Mashtaka na maafisa wanaotekeleza majukumu kwa niaba yake wakati wa kutekeleza majukumu yao ambayo ni; nia ya kutenda haki, kuzuia matumizi mabaya ya taratibu za utoaji haki na kuzingatia maslahi ya umma.
3. Kifungu cha 9(1) (c) cha Sheria ya Usimamizi wa Mashtaka, Sura ya 430 kinampa Mkurugenzi wa Mashtaka mamlaka ya kusimamia na kuratibu upeletelezinaofanywa na vyombo chunguzi ili kuhakikisha unazingatia sheria na unakuwa na tija katika uendeshaji wa mashtaka.

SEHEMU YA PILI
MADHUMUNI YA MWONGOZO

4. Madhumuni ya mwongozo huu ni kutoa mwongozo wa kuzingatia katika ukamilishaji wa upelelezi wa kesi za jinai na wakati wa ufunguaji mashtaka mahakamani.
5. Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai Sura ya 20 imefanyiwa mabadiliko kuititia Sheria ya Mabadiliko ya Sheria (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act) Namba 1 ya mwaka 2022. Mabadiliko yaliyofanywa ni pamoja na kuongezwa kifungu kipyaa cha 131A kinachohusu ufunguaji wa mashtaka Mahakamani katika Mahakama za Hakimu Mkazi na Mahakama za Wilaya.
6. Katika mabadiliko hayo, Sheria imeweka masharti ya lazima ya upelelezi kukamilika kwanza kabla ya mashtaka kufunguliwa Mahakamani kwa makosa yote isipokuwa makosa makubwa (serious offences) ambayo yanahusisha makosa ya unyang'anyi wa kutumia silaha, usafirishaji haramu wa binadamu na dawa za kulevyaa, umiliki wa nyara za Serikali isivyo halali na makosa mengine yanayosikilizwa na Mahakama Kuu. Sheria imeelekeza zaidi kuwa kwa makosa mengine kama upelelezi haujakamilika mtuhumiwa anatakiwa kupewa dhamana ya Polisi.

UTARATIBU WA KUKAMILISHA UPELELEZI NA UFUNGUAJI WA MASHTAKA

7. Kwa kuzingatia marekebisho tajwa katika Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai, Sura 20 katika kifungu cha 131A sanjari na changamoto ambazo zimeendelea kujitokeza katika ukamilishaji wa upelelezi, Mwongozo huu unaelekeza yafuatayo:

- i. Wakuu wa Mashtaka wa Mikoa, Wilaya, Waendesha Mashtaka Viongozi na vyombo vyote vya uchunguzi vinavyohusika na ufunguaji wa Mashtaka wahakikishe kifungu cha 131A cha Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai Sura ya 20 kinazingatiwa;
- ii. Kesi zote ambazo chini ya kifungu 131A zimeelekezwa kufunguliwa upelelezi wake ukiwa umekamilika muhakikishe hoja za awali ziandaliwe na kusomwa mahakamani wakati kesi inapofunguliwa;
- iii. Kwa kesi ambazo zimeruhusiwa kisheria kufunguliwa upelelezi ukiwa haujakamilika muhakikishe kwamba upelelezi wa kesi hizo unakamilika ndani ya kipindi kisichozidi siku tisini (90) bila kuathiri maelekezo ya Mkurugenzi wa Mashtaka katika Mwongozo wa ufunguaji wa Mashtaka na ukamilishaji wa Upelelezi wa kesi za Jinai wa tarehe 24 Machi, 2022;
- iv. Kesi yoyote ambayo kuna sababu ya msingi kwa upelelezi wake kuchukua zaidi ya siku 90, Mkuu wa Mashtaka wa Mkoa anatakiwa kuomba kwa maandishi kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kibali cha kuongezewa muda wa kukamilisha upelelezi bila ya kuathiri taratibu na sheria zinazosimamia ukomo wa upelelezi kwa baadhi ya makosa. Kibali hicho cha kuongeza muda kitaombwa kabla ya muda wa siku (90) kukamilika;
- v. Watuhumiwa ambao matakwa ya sheria yanataka wafikishwe mahakamani baada ya upelelezi wa tuhuma dhidi yao kuwa umekamilika wapewe dhamana za Polisi wakati wakisubiria kukamilika kwa upelelezi;
- vi. Ukaguzi wa mahabusu za polisi ufanyike kila wiki kuhakikisha watuhumiwa hawashikiliwi muda mrefu wakati wanasubiri kupelekwa mahakamani.

**SEHEMU YA TATU
UTEKELEZAJI WA WARAKA**

8. Wakuu wa Mashtaka wa Mikoa, Wilaya, Waendesha Mashtaka Viongozi na Wakuu wote wa vyombo vya uchunguzi wanapaswa kutekeleza na kusimamia maelekezo ya mwongozo huu.
9. Mwongozo huu utaanza kutumika tarehe 01 Oktoba, 2022.

Umetolewa Dodoma tarehe 30 Mwezi Septemba, 2022



**Sylvester Antony Mwakitalu
MKURUGENZI WA MASHTAKA**